


## Ujifunzaji wa Kitaaluma kwa ajili ya Walimu kuboresha Upekeeshaji

Tafiti zinaonyesha mara kwa mara kwamba walimu ni muhimu zaidi katika ujifunzaji wa mwanafunzi zaidi ya mikakati mingine ya kusaidia elimu. Tukiwa na lengo la kupunguza ukosefu wa usawa kupitia elimu, TeachUNITED inatumia ujifunzaji wa kitaaluma kama mbinu mkakati katika kuleta matokeo makubwa kwa wanafunzi wengi.

Uwezo mkubwa wa walimu darasani una matokeo chanya katika kusaidia wanafunzi kufanya vizuri kitaaluma, kufanikiwa kuingia vyuoni, na hatimaye kupata mapato katika shughuli zao za baadaye.<sup>1</sup> Kadri uwezo wa mwalimu unavyoongezeka ndivyo wanafunzi wenye uwezo mdogo darasani wanavyokuwa wa kwanza kunufaika. Matokeo ya ubora wa mwalimu katika mafanikio ya mwanafunzi ni endelevu, ikimaanisha kwamba kiwango cha mafanikio ya mwanafunzi kinaweza kuathiriwa na mwalimu mwenye uwezo wa juu kwa miaka mingi ijayo.

### Matokeo ya Ubora wa Mwalimu katika Utendaji wa Mwanafunzi



Ubora wa mwalimu ni muhimu pia kwa mahudhurio ya wanafunzi, kusimamishwa shule, kufuatilia maendeleo ya daraja (grade) kwa wakati, na uwezo wa kijamii na kihisia wa mwanafunzi.<sup>2</sup> Zaidi ya hayo, matokeo ya wakufunzi wenye uwezo sanifu wa juu unaenda zaidi hadi kwa wanafunzi ambao hawafundishwi nao. Kama Opper anavyosema, walimu wanaleta matokeo kwa wanafunzi kupitia ufundishaji, shughuli za ziada, na kwa kuleta mabadiliko kwa walimu wenzao shuleni.<sup>3</sup> Walimu wanapojifunza kupitia wao, mwalimu bora anaweza kuleta matokeo kwenye mafanikio ya kielimu kwa wanafunzi ambao hawapo kwenye madarasa yake.

<sup>1</sup> Sanders & Rivers (1996): Cumulative and Residual Effects on Future Student Academic Achievement, Knoxville, TN: Univ of Tennessee.

<sup>2</sup> Doan, S. (2019). Beyond Achievement: How Teachers Affect Outcomes Other than Test Scores. Santa Monica, CA: RAND Corporation.

<sup>3</sup> Opper, I.M. (2019) Teachers Matter: Understanding Teachers' Impact on Student Achievement, Santa Monica, Calif.: RAND Corporation, RR-4312.



## Msingi wa TeachUNITED katika Ujifunzaji wa Kitaaluma

Kwa vile wakufunzi wana mchango mkubwa sana katika matokeo ya wanafunzi, School Accelerator Program (SAP) inalenga katika mikakati ya ufundishaji ambayo inaleta matokeo makubwa kwa mwanafunzi. Zifuatazo ni tafiti zinazosaidia School Accelerator Program (SAP).

1. Usawa kulingana na uwezo wa kila mwanafunzi: Mikakati ya Ufundishaji, Utamaduni wa Darasa, Kutengeneza Mazingira ya Mafanikio kwa Wote.
  - a. Carol Dweck - Growth / Fixed Mindset
  - b. John Hattie - Visible Learning & Meta-Analysis of Teacher Effect
  - c. Jim Knight - High Impact Coaching Cycle
  - d. Phillip Schlechty - Student Engagement Strategies
2. Utafiti wa Ujifunzaji wa Kipekee & Mchanganyiko (Personalized & Blended Learning)
  - a. Organizations - ISTE, iNACOL, Evergreen Consulting
  - b. Katherine Kennedy & John Watson, Digital Learning Collaborative
  - c. Jal Mehta & Todd Rose, Harvard and Justin Reich, MIT
  - d. Allison Zmuda, ASCD Understanding by Design Cadre
  - e. John Pane and Bob Murphy, RAND
  - f. Barbara Means, Digital Promise
  - g. Tom Vanderark, Getting Smart

## Mafunzo kwa ajili ya Uwasilishaji na Ubunifu wa Mafunzo ya Kitaaluma

Kuna makubaliano mapana ya jumla kwa watafiti kuhusiana na nini kinafanya mafunzo ya kitaaluma kuwa bora. Mafunzo bora ya kitaaluma yanahitaji fursa endelevu za kujifunza na ujifunzaji hai, uundaji wa mfano, majadiliano mapana, na fursa za vitendo.<sup>4</sup> Mafunzo bora ya kitaaluma yanatakiwa yajumuishe fursa nzuri za kushirikiana na kushiriki kwa pamoja, ambayo inasaidia mshikamano mkubwa katika maendeleo, na ujifunzaji hai zaidi kwa wanataaluma.<sup>5</sup> Unapoangalia vigezo vya Mafunzo ya Kitaaluma bora, ukufunzi lazima uwe msingi wa Programu yoyote iliyofanikiwa.

**“Mchanganuo wa matokeo kutoka tafiti 60 zimeonyesha kuwa ukufunzi unafanya kazi. Kupitia ukufunzi, ubora wa ufundishaji wa walimu unaongezeka zaidi ya utofauti wa ubora kati ya mwalimu mpya kwenye taaluma na mwalimu mwenye miaka 5-10 kwenye taaluma, haya ni matokeo mazuri kabisa kukadiriwa Zaidi ya mafunzo ya kitaaluma ya zamani, na mikakati mingine mingi ya shule”<sup>6</sup>**

<sup>4</sup> Hill, H. C., Beisiegel, M., & Jacob, R. (2013). Professional development research: Consensus, crossroads, and challenges. *Educational researcher*, 42(9), 476-487.


<sup>5</sup> Garet, M. S., Porter, A. C., Desimone, L., Birman, B. F., & Yoon, K. S. (2001). What makes professional development effective? Results from a national sample of teachers. *American educational research journal*, 38(4), 915-945.

<sup>6</sup> Blazar, David; Kraft, Matthew A., *Education Next* - Fall 2018 Vol 18 No.4, 2018.

Watafiti wa Stanford Graduate School of Education waligundua mambo manne kama ifuatavyo;

1. Muda na Mgawanyiko: Ujifunzaji wa Kitaaluma unatakiwa udumu kwa muda mrefu ili kusaidia utekelezaji bora.
2. Ufundishaji Mahiri na Ushirikiano: Mafunzo endelevu na ushirikiano kati ya walimu na wakufunzi kupitia uchunguzi, mrejesho, na uchambuzi wa data.
3. Mafunzo ya Vitendo: Ujifunzaji hai ambapo walimu wanapata fursa ya kufanya kwa vitendo na kutendea kazi walichojifunza.
4. Teknolojia: Mfumo bora wa kujifunza kidijitali ni bora na sanifu zaidi kama mafunzo yasiyofanyika kwa njia ya mtandao, pia mafunzo ya kidigitali yanawezesha upekee wa muda, mada, na utayari wa kujifunza.<sup>7</sup>

## Asmilimia ya Walimu Wanaotekeleza Ujuzi Mpya



## Kulinganisha Matokeo Ya Ujifunzaji Wa Kitaaluma Kupitia Njia ya Mtandao na Njia ya Ana kwa Ana

UVIKO-19 ilibadilisha mifumo ya kielimu kwa haraka kuelekea kwenye njia ya mtandao, na mafunzo mchanganyiko katika ujifunzaji wa kitaaluma. Hata hivyo njia ya mtandao, na njia ya mchanganyiko (mtandao na ana kwa ana) katika Ujifunzaji wa Kitaaluma ulianza kabla ya janga la UVIKO-19 na tafiti zimekuwa zikionyesha njia hii inaweza kuwa bora kama ile ya ana kwa ana katika Ujifunzaji wa Kitaaluma. Jarida la Teacher Educator mwaka 2013 lililinganisha Ujifunzaji wa Kitaaluma kwa njia ya mtandao na ule wa ana kwa ana na kugundua kuwa walimu na wanafunzi walionyesha matokeo muhimu katika njia zote, na kwamba hakukuwepo na utofauti wa kimatokeo. Ujifunzaji wa Kitaaluma kwa njia ya mtandao unatoa uchaguzi/machaguo mengi, na shule zilizopo mbali zinaweza kupata mafunzo mbalimbali na katika njia rahisi zaidi.<sup>8</sup>

<sup>7</sup> Ball, A.F. (2015). Effective professional development for 21st century learning [research paper]. Stanford, CA: Stanford University of Education.

<sup>8</sup> Bates, M. S., Phalen, L., & Moran, C. (2016). Online professional development: A primer. Phi Delta Kappan, 97(5), 70-73.